



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA MANISPAA YA LINDI



TANGAZO NAFASI YA KAZI YA MKATABA

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Manispaa ya Lindi, anapenda kuwatangazia wataanzania wenye sifa kuomba nafasi ya kazi ya mkataba ifuatayo:

AFISA HABARI DARAJA LA II (Nafasi 1)

SIFA:

- Awe na shahada ya kwanza au inayolingana kutoka chuo kinachotambulika na serikali katika fani ya Uandishi wa Habari na Utangazaji wa Umma.
- Awe na umri kuanzia miaka 18-44
- Awe Mtanzania
- Awe anajua kutumia kompyuta pamoja na Mitandao ya Kijamii

MAJUKUMU YA AFISA HABARI DARAJA II

- Kukusanya, kuhariri, kuandika na kutoa habari za uhakika kwa jamii
- Kuchukua picha jongefu na mnato za matukio mbalimbali ya Manispaa
- Kuweka kumbukumbu wa matukio kwa njia ya picha
- Kuendesha mitandao ya kijamii inayomilikiwa na Manispaa ikiwemo website, Instagram, Twitter na Facebook.
- Kuandaa makala za habari, vipeperushi, na kukusanya taarifa za kitakwimu za Manispaa na kuzisambaza kwa wananchi kwa njia ya habari.

MSHAHARA:

Malipo ya mshahara yatakuwa ni makubaliano ya pande mbili.


JINSI YA KUOMBA:

Maombi yawasilishwe yakiambatana na vyeti halisi vya elimu na taaluma pamoja na wasifu (CV), cheti cha kuzaliwa, kitambulisho cha NIDA, picha ndogo mbili (passportSize) pamoja na namba za simu.

Maombi yanaweza kuletwa kwa mkono au Posta kwa anuani ya:

Mkurugenzi wa Manispaa,
S.L.P 1070,
LINDI

Mwisho wa kupokea maombi na tarehe 29.9.2023 saa 9.30 alasisi.


Juma Mtwale
Mkurugenzi wa Manispaa,
LINDI.

MKURUGENZI WA MANISPAA
LINDI